MUSWADA WA TAMADUNI TOFAUTI VICTORIA 2011
HOTUBA YA PILI
MHESHIMIWA. NICHOLAS KOTSIRAS, MBUNGE

Nashauri Muswada huu usomwe kwa mara ya pili.

Serikali inatambua kuwepo kwa tamaduni tofauti hapa Victoria, na itatekeleza mipango ambayo itawezesha Victoria kuendelea kuongoza majimbo mengine hapa nchini kwenye masuala yanayohusiana na tamaduni tofauti. Muswada wa Tamaduni Tofauti 2011 (the Multicultural Victoria Bill 2011) utatekeleza jambo mojawapo muhimu kuhusiana na hili kwa kubadilisha Tume ya Tamaduni Tofauti Victoria iliyopo hivi sasa na kuanzisha chombo kipya chenye nguvu na mamlaka huru ya kisheria.

Tume hiyo ni chombo muhimu Serikalini katika kamati inayotoa ushauri kuhusiana na masuala yanayohusiana na tamaduni tofauti na vilevile ni chombo kinachounganisha wanajumuia za Victoria na Serikali ya Victoria. Ninaimani kuwa jambo la kwanza na muhimu ni kuwa ni sauti inayowakilisha Victoria kwenye masuala ya tamaduni, dini, rangi na lugha mbalimbali. Ndani ya Muswada, jambo hili linawakilishwa kwa kutumia msamiati wa mchanganyiko wa mila "diversity".

Utangulizi wa Muswada

Muswada unawasilisha ahadi ya Serikali kupanga na kuimarisha kitengo kinachohusiana na mambo ya tamaduni tofauti, ikijumuisha Tume ya Tamaduni Tofauti Victoria. Muswada huo utafanikisha malengo yake kwa namna tatu:

- Moja, Muswada utaongeza uhuru wa Tume kwa kuanzisha chombo kipya cha kisheria. Chombo hicho kipya kitaendelea kutumia jina la Tume ya Tamaduni Tofauti Victoria (the Victorian Multicultural Commission), lakini italenga zaidi katika kuimarisha jamii yetu. Uhuru wa Tume utaongezeka kwa kuwa na nguvu ya kisheria kufanya utafiti wa kitaalam, kutoa ripoti na kumshauri Waziri moja kwa moja kuhusiana na masuala ya mfumo wa kijamii kuhusiana na Tume. Masuala hayo yanaweza kutambuliwa na Mabaraza ya Ushauri Mikoani au kupitia njia nyengine za mawasiliano na jamii, au kuhusiana na upungufu wa huduma za serikali, usaidizi wa makazi na utoaji huduma kwenye jamii mbalimbali.
- Pili, Muswada huu utaimarisha muungano kati ya Serikali na Jumuia mbalimbali za Victoria kupitia Mabaraza ya Ushauri Mikoani.
- Tatu, Muswada unatambua ushiriki wa Serikali yote katika masuala ya Tamaduni Tofauti kwa kupitia kifungu mahususi.

Kuongezea, Muswada huo (the Multicultural Victoria Bill 2011) unachukua nafasi ya sheria iliyopita *Multicultural Victoria Act 2004* kwa:

- Kuendeleza misingi ya tamaduni tofauti;
- Kuongeza malengo na kazi za Tume mpya; na
- Kuendelea kutoa ripoti kuhusiana na mahitaji kwa ajili ya Idara za Serikali kuhusiana na masuala ya Tamaduni Tofauti.

Tume ya Tamaduni Tofauti Victoria(Victorian Multicultural Commission)

Kuanzishwa kwa tume huru ya Tamaduni Tofauti Victoria kutatengeneza muunganiko mzuri baina ya Serikali na Jumuia mbalimbali za Victoria.

Tume mpya italenga katika kutoa usaidizi kwa wanaVictoria na nategemea itatoa ushauri kwa uwazi na bila woga/hofu kwa Serikali.

Tume itafanikiwa kuwa huru kwa mujibu wa sheria na utendaji mpya ambao utawezesha kutoa ushauri moja kwa moja kwangu, kama Waziri mhusika, kuhusiana masuala yatokanayo na mfumo na upatikanaji wa nafasi kwenye jamii mbalimbali.

Tume mpya itakuwa na majukumu ya ziada kufanya tafiti, kutoa ushauri na kutoa taarifa kwangu, kama Waziri mhusika. Majukumu hayo yanaweza kuanzishwa na Tume au mimi kuomba.

Ili kufanikisha uandaaji na utoaji ripoti wa Tume, Viongozi wa Wizara watakaofuatwa na Tume kwa ajili ya taarifa itawabidi wahakikishe nguvu zote ziwezekanavyo zitumike kusaidia Tume kufanya utafiti wake.

Makamishna kumi na mbili watachaguliwa na Gavana wa Jimbo kujiunga na Tume mpya, itajumuisha:

- Mwenyekiti atakayefanya kazini muda wote;
- Makamu Mwenyekiti atakayekuwa kazini si muda kamili;
- Makamishna nane watakaokuwa wanafanya kazini si muda kamili watakaokuwa na ujuzi na utaalam unaotakiwa;
- Mwakilishi wa vijana atakayefanya kazini si muda kamili; na
- Mwakilishi wa kikundi cha jamii ambaye mimi nitamchagua.

Tume mpya itakuwa huru kutoka kwenye Wizara za Serikali na Mwenyekiti wa Tume atakuwa na mamlaka ya kuajiri wafanyakazi na kuingia mikataba. Wafanyakazi wataajiriwa kama wafanyakazi wa umma na watakuwa wakifuata muongozo wa Victorian Public Sector Code of Conduct.

Mabaraza ya Ushauri Mikoani

Muswada unatoa mwongozo wa kuanzishwa kwa Mabaraza nane ya Kutoa Ushauri katika maeneo ya mikoani hapa Jimboni. Mabaraza yatafanya kazi kwa ukaribu na jumuia tofauti kwenye maeneo hayo na yatakuwa kiunganishi muhimu kutoa taarifa kuhusiana na masuala yanayohusiana na majukumu ya Tume ikijumuisha makazi ya kudumu mikoani na utoaji huduma.

Kila mmoja wa Makamishna nane watakaokuwa wanafanyakazi atakuwa mwenyekiti wa Baraza La Ushauri, itawasaidia kutumia ufahamu na ujuzi wa maeneo yao kutoa njia kwa Serikali kufahamu masuala yanayotatiza jamii mbalimbali za wakazi wanaoishi mikoani, inajumuisha ushauri kuhusiana na ufanisi na upatikanaji wa huduma za Serikali na usaidizi wa kuhusiana na makazi.

Wakati haijaandikwa kwenye Muswada, inategemewa kuwa Mabazara ya Ushauri Mikoani yatakuwa na majukumu yafuatayo:

- Kwanza, Mabaraza ya Ushauri Mikoani yatatumia ufahamu na uelewa wa wakazi wa kwenye jumuia kutoa ushauri kwa Tume kuhusiana na matatizo na utoaji wa nafasi kwa wakazi wenye tamaduni tofauti, mkazo zaidi ukiwa kwenye ufanisi na upatikanaji wa huduma za Serikali na usaidizi wa makazi.
- Pili, Mabaraza yatashirikia na biashara, waajiri na maofisa wanaosaidia maendeleo ya biashara ili kusaidia kufungua njia mpya za upatikanaji wa kazi na kutangaza maeneo ya mikoani Victoria kuwa ni maeneo mazuri kwa waamiaji wapya kuweka makazi ya kudumu

- Tatu, Mabaraza yataandaa makongamano/mikutano mikoani, na kutoa nafasi kusherehekea mchango inayotokana na mila na dini tofauti hapa Victoria, na kuchangia mahusiano mazuri kwenye jamii.

Mahitaji ya Uandaaji Ripoti katika Wizara za Serikali
Chini ya Muswada, Wizara za Serikali zitahitajika kuandaa na kutoa ripoti kwangu, kama Waziri mwenye dhamana, kwenye kila kalenda ya mwaka wa fedha kuhusiana na na jinsi gani Wizara imechangia au kwa namna gani imesaidia jamii zenye tamaduni tofauti zilizopo Victoria. Hii inaendana na wajibu wa Muswada uliopita *Multicultural Victoria Act 2004*.

Misingi ya Tamaduni Tofauti
Serikali inatambua kuwa uraia wa Australia ni kigezo cha kujenga jamii imara na iliyoshikamana, ambapo kila mmoja anajifunza kutoka kwa mwenzie na kwa pamoja inasaidia kuleta jamii inajumuisha wote bila vurugu. Suala la uraia kwenye Muswada haliishi kwenye uraia rasmi wa Australia, lakini inajumuisha haki na wajibu wa watu wote kwenye jamii yenye tamaduni tofauti. Suala la uraia linaunganisha jumuia tofauti kwenye jamii katika kujitolea kujenga nchi yetu na vyombo vya kidemokrasia, sheria, vinavyotuongoza na dhana ya ‘fair go’.

Muswada utarudisha nguvu mpya za maadili ya tamaduni tofauti yanayojumuisha misingi ya uraia, kuthamini majukumu ya pamoja kwa Australia na kwa huduma za jamii, na kutambua mchanganyiko wa mila ni rasilimali kwa Victoria. Muswada pia unaeleza kuwa Bunge lisaidie kwenye masuala ya uraia na mchanganyiko wa tamaduni kwa kutambua misingi ya tamaduni tofauti, inayojumuisha kuheshimiana na maelewano, kukuza mila tofauti na urithi, na kutoa nafasi na kushiriki. Kanuni za tamaduni tofauti zinasaidia kuunda jamii iliyona amani na yenye ushirikiano.

Mwisho
Muswada mpya wa Tamaduni tofauti (The new Multicultural Victoria Bill) 2011 utasaidia kuhakikisha kwamba huduma zinazotolewa na Serikali ya Victoria zinafikia kiwango kinachotegemewa na jamii yetu inayozidi kuwa na tamaduni na mila tofauti, na huku sauti za jumuia zetu zikizidi kusikika kwa ufasaha.

Muswada utahimarisha muelekeo wa Victoria kwenye masuala yanayohusu Tamaduni tofauti na uraia, kuweka msingi wa kujenga jamii imara na yenye nguvu.

Nawasilisha Muswada huu bungeni.